Mawazo ya Biashara

Tutaanzisha na kusimamia biashara mbalimbali za shughuli za metali na uchimbaji madini tukiwa na lengo moja tu la kuwapatia wanahisa wetu manufaa makubwa kiviwanda. Tutaweza tu kuyafanikisha haya kwa kujenga ushirikiano wa dhati baina yetu na wafanyakazi, wateja, wanahisa, jamii za wenyeji wetu pamoja na wadau wengine; ushirikiano ambao misingi yake ni uadilifu, ushirikiano, uwazi na utengenezaji wa pamoja wa thamani au faida.

1 Tamko kutoka kwa Afisa Mkuu Mtendaji
2 Tunafanya kazi kwa Maadili
3 Tunafanya kazi kwa Majukumu
4 Tunafanya kazi kwa uwazi
5 Tunafanya kazi kwa pamoja na wengine
6 Mawasiliano na wafanyakazi
Maulizo ya nje

Kauli hii ya mawazo ya biashara inatumika katika kila tendo linalosimamiwa na Xstrata. Matendo yasiyosimamiwa na ambayo Xstrata inajihusisha nayo yanahitajika kuwa na sera na sheria ambazo zinakaribiana na mawazo haya.

Mawazo yetu ya biashara ndiyo yanayokariri maadili na nyendo kwa kila mmoja ambaye Xstrata inapendekeza. Yanaungwa mkono na kujitolea kwa njia maalumu-, matarajio na miongozo inayowekwa wazi katika sera zetu, viwango vya maendeleo endelevu na taratibu.

Tamko kutoka kwa Afisa Mkuu Mtendaji

Tumeajiriwa na wamiliki wa Xstrata ili kuwatengenezea thamani au faida kutokana na Uwekezaji wao. Kauli ya Dhamiri yetu inabainisha changamoto yetu na inaweka wazi kabisa kwamba mafanikio yanawezekana tu kupitia kuanzisha na kuendeleza ushirika wa ukweli na wadau wetu; ambao una sifa za uadilifu, ushirikiano, uwazi na utengenezaji wa pamoja wa thamani au faida.

Kanuni za Kikazi za Xstrata zinaenda hatua moja mbele na kutafsiri Dhamiri yetu kwa namna tunavyofanya kazi.

Hapa Xstrata, tunatoa majukumu makubwa zaidi na mamlaka katika biashara zetu za bidhaa ulimwenguni huku tukihifadhi Kituo kidogo cha kikampuni na tukipunguza mzigo wa gharama. Ninaamini kwa dhati kwamba muundo huu wa usimamizi wa kipekee unayafaida matendo yetu na wadau wetu kwa njia ya moja kwa moja kwa kuunda hali kubwa ya umilikaji na uwajibikaji katika kiwango cha ndani kwa ndani. Kwa maana zimewezeshwa kutenda, biashara zetu zinaweza kuhusishwa na wadau wa ndani na kuwaitikia vilevile, changamoto na fursa kwa njia ifaayo zaidi-ni hitaji la muhimu lililopewa upana unaohusihwa na matendo yetu ulimwenguni.

Hata hivyo, makundi mengi makubwa yasiyojulikana ndani ya biashara zetu za bidhaa, yamefungwa pamoja na nidhamu na imani kuhusu namna tunavyofanya kazi, yote ambayo yameandikwa katika tamko hili la Mawazo ya Biashara. Hususani, kanuni hizi zinatambua kwmaba kujitolea kwetu katika ushirikiano wa ukweli na wadau wetu kunahitaji kwamba:

– tufanye kazi kiuadilifu
– tufanye kazi kiuwajibikaji
– tufanye kazi kiuwazi na
– tufanye kazi pamoja na wengine

Changamoto yetu hasa ni kuhakikisha kuwa malengo haya yanaoonekana katika matendo yetu ya kila siku, mitazamo yetu na maamuzi yetu. Ili hayo yaweze kutimia, kila mmoja wetu sharti alichukue jukumu la kibinafsi katika kutekeleza mambo hayo kwenye sehemu ile ya biashara ambayo tunalo jukumu nayo na kwa kuendeleza matumizi yake na washirika wetu wa kibiashara, wakiwa ni pamoja na washirika wetu wa kikazi na wanakandarasi.

Ni jukumu la kila mmoja kutoa maoni yake kuhusu mambo yoyote yanayohusu kukubaliana na mawazo ya biashara, kwa hali ya kwanza kupitia meneja mhusika.'Mstari wa maadili' usiojulikana na uendeshwao kwa uhuru unatolewa pia katika kila nchi ambayo Xstrata hufanyia kazi. Hali hii ni kwa wakati ule ambapo hali hii haiwezekani na maelezo yametolewa katika upande wa nyuma wa jalada la makala haya.

Kanuni zetu za kazi hazikusudiwi kufanya kazi kama sheria elekezi za shirika. Aidha, hazitarajiwi kubainisha majukumu mahususi tukiwa kazini. Yanakariri kuwajibika baina yetu na kwa wadau wetu katika kuonyesha jinsi tutakavyofanya kazi. Mawazo haya yetu ya biashara yanatoa muundo wa kimaadili na sehemu ya kurejelea kwa utamaduni wetu wa kikampuni, kwa biashara za Xstrata kote ulimwenguni ambako mtazamo kamili katika kuangalia thamani unamaanisha kujitolea kusikolegezwa katika tabia ya kimaadili na ya uwajibikaji.

Ninafahari kwa utamaduni wa kampuni ndani ya Xstrata ambapo mtazamo wetu katika uundaji wa thamani kwa kundi la wamilikaji unahusishwa moja kwa moja na kujitolea kwetu katika kufikia viwango vya juu zaidi vya nidhamu na uwazi. Bila kuficha ni muhimu kusema kwamba, licha ya tamaduni mbalimbali, mila na sheria ambazo tunatendea kazi mawazo yetu hayafai kulegezwa kamwe.

M L Davis, Afisa Mkuu Mtendaji, Xstrata plc

Tunafanya kazi kwa Maadili

Tumejitolea kuwa na viwango vya juu zaidi vya maadili ya kibinafsi na kitaalam wakati wote.

Tunafanya mambo kwa nidhamu na heshima katika uhusiano wetu na wadau na kutimiza ahadi zetu na majukumu yetu kwao.

Tunatii kwa ukamilifu sheria na masharti katika kila nchi ambayo tunatendea kazi. Mbali na hayo, tunatenda kazi kwa kuambatana na muundo wa Xstrara wa maendeleo endelevu, huku tukilenga kufikia viwango vya juu zaidi vya kimataifa licha ya mahali na bila ya kuacha chochote.

Tunahitaji wabia wetu wa biashara kushikilia mawazo ya biashara ya Xstrara, sera na viwango vya maendeleo endelevu.

Tunashikilia na kuziendeleza haki za binadamu ndani ya maeneo yetu ya uwezo huku tukiheshimu asili ya utamaduni, mila na haki za jamii, pamoja na wenyeji.

Hatutoi, kuomba wala kukubali mfumo wowote wa hongo au chochote ambacho kinaweza kudhaniwa kwamba ni hongo.

Hatutoi michango kwa chama cha kisiasa, shirika la kisiasa, mwanasiasa au mtu aliye na ofisi ya umma.

Hatuvumilii njia yoyote ya ulaghai, pamoja na wizi na matumizi yasiyofaa ya rasilimali ya kampuni kwa faida ya kibinafsi.

Haturuhusu mapendeleo yetu ya kibinafsi ya kifedha kugonganishwa na mapendeleo ya kampuni.

Tunaunga mkono hali huru ya kibiashara na tutashindania kwa usawa biashara mbalimbali, kwa kutilia maanani sana sheria zile zinazoendeleza ushindani na kuwalinda watumiaji.

Tunaheshimu kandarasi zote tunazopanga na wagawaji na wateja wetu na tunalipia viwango vizuri vya kibiashara kwa bidhaa na huduma.

Tumejitolea katika utawala wa kikampuni ulio wa kipekee na unaowajibikiwa.

Tunafanya kazi kwa kuwajibika

Tumejitolea kufikia katika lengo la Maendeleo endelevu. Tunasawazisha mazingatio ya kijamii, kimazingira na uchumi kwa jinsi ambavyo tunavyosimamia biashara yetu.

Tunatambua na kusimamia hatari za kifedha, kimatendo, za afya, usalama, kimazingira, kisiasa na kimazoea katika biashara yetu ili kutuwezesha kufuatilia fursa mbalimbali kwa moyo wa kijasiriamali.

Tunatoa uongozi unaonekana; mazingatio yanayoeleweka, makusudio na malengo; na rasilimali zifaazo za kifedha na kibinadamu ili kufikia makusudio yetu kabambe.

Tunatekeleza mikakati, sera, viwango, mifumo na taratibu ili kufikia makusudio yetu ambayo yanatekelezwa na kuwekwa sambamba kati ya kundi, biashara ya bidhaa na viwango vya kutenda kazi.

Tunalenga katika kufanya kazi katika mahali pa kazi salama ambapo hapana majeraha na balaa na kusisitiza hali nzuri ya waajiriwa, wanakandarasi na jamii.

Tunalo jukumu la usalama wetu na hali yetu nzuri na kwa usalama na hali nzuri ya wengine walio karibu nasi katika mahali petu pa kazi na katika jamii.

Tunafanya kazi tukiwa viongozi wenye jukumu la kuilinda mali ya wamiliki wetu na tunalenga kuhifadhi afya ya kipindi kirefu, umuhimu na ubora wa mazingira ya kawaida ambayo yanaathiriwa na matendo yetu.

Tunalenga katika uboreshaji wa siku zote katika kila hali ya biashara yetu.

Tunafanya kazi kwa uwazi

Tumejitolea kuwa na uwazi mkubwa ambao unawezekana kibiashara katika biashara yetu.

Tunatoa ripoti mara kwa mara kwa umma kuhusu utendakazi wetu wa kifedha, kimatendo, na maendeleo endelevu. Haya yote yanaambatana na sheria zote zifaazo na viwango vya utendakazi vinavyoongoza.

Tunatoa ripoti ya taarifa ya utendakazi wa kifedha na kibiashara kwa ukamilifu, uyakinifu, ukweli, na kwa muda ufaao.

Tunawasilisha mapema athari zinazowezekana na faida za mabadiliko yote makubwa yaliyopendekezwa katika matendo yetu, miradi au shughuli kwa wadau wote wahusikao kwa uwazi, ujumla na njia ifaayo ya kitamaduni.

Tunawatumia wataalam wa kuaminika, na waliohuru ili kukagua na kutoa uhakikisho wa mifumo yetu ya usimamizi na utendakazi wa biashara katika viwango vya kundi, biashara ya bidhaa na kimatendo.

Mara kwa mara sisi huweka kiwango chetu dhidi ya viwango vya kimataifa na matendo yanayoongoza pamoja na jukumu la kulina utendakazi unaoongoza viwandani.

Tunafanya kazi kwa pamoja na wengine

Tumejitolea kuwa na ushirikiano wazi na wa makubaliano na waajiriwa, wawakilishi wa waajiriwa, wateja, wagawaji wa hisa na wadau.

Tunatambua wadau katika shughuli zetu na kuwasiliana nao kwa ukweli pamoja na kushirikisha kwa nia njema makundi yote ya wadau.

Tunaendeleza utendakazi wa kiwango cha juu na utamaduni wa kijasiriamali pamoja na kuonyesha majukumu ya juu zaidi na mamlaka kwa biashara zetu za bidhaa ulimwenguni na shughuli mbalimbali, kuingiza umilikaji katika kiwango cha kitaifa.

Tunalenga kuwavutia na kuwahifadhi watu bora zaidi katika kila kiwango cha biashara na kutoa fursa za maendeleo ya ajira zitakazoongoza viwandani kote.

Tunauthamini mchango unaofanywa na waajiriwa na wanakandarasi, na sera zetu pamoja na shughuli zinaheshimu utu na haki zao za kibinafsi.

Kwa namna mbalimbali tunawathamini na kuwatendea sawa wafanyakazi wetu wa kudumu na wale wa mkataba, tunatoa fursa sawa kwa wote katika ngazi zote za shirika bila ubaguzi wa rangi, utaifa, udini, jinsia, umri, ulemavu, kisiasa kwa jambo au misingi yoyote ile mingine.

Tunatambua na kushikilia haki za wafanyakazi wetu na kuwapa mahali pa kazi penye usalama, uwakilishwaji wa jumla, ulipwaji fidia sawa, usalama wa kazi na fursa za maendeleo.

Hatuendelezi wala kuvumilia mfumo wowote wa ubaguzi katika mahali pa kazi, upigwaji, unyanyaswaji au uumizwaji wa mwili.

Hatuendelezi wala kuvumilia ajira ya mtoto au mfumo wowote wa kuajiririwa kwa lazima au kwa masharti katika Xstrata au wabia wetu wa biashara.

Tunafanya kazi na serikali, mamlaka ya majiji, wawakilishaji wa jamii, mashirika ya kiserikali na yasiyokuwa ya kiserikali pamoja na wote wanaohusika ili kuendeleza na kuunga mkono miradi inayofaidi jamii zinazohusiana na shughuli zetu ulimwenguni.

Tunachangia katika maendeleo ya kijamii na kiuchumi ya jamii endelezi zinazohusishwa na shughuli zetu.

Tunaheshimu tamaduni, mila, mapendeleo na haki za jamii, wakiwamo wenyeji na makundi dhaifu au yaliyowahi kuhasiriwa.

Tunaanzisha kwa kasi uhusiano na wadau wetu katika kiwango cha kimataifa, kitaifa, kimaeneo na kieneo na tunatafuta msaada mpana na unaoendelea kwa minajili ya shughuli zetu kutoka jamii zinazohusishwa na shughuli zetu.

Tunafanya kazi na wateja wetu, wagawaji, wanaviwanda wenzetu na vyama ili kuboresha utendakazi wa jumla wa viwanda na kupunguza athari za kimazingira au afya zinazohusishwa na bidhaa zetu.

Mawasiliano na Wafanyakazi
Kila mfanyakazi na mkandarasi wa Xstrata ana wajibu wa kufanya kazi kwa kuzingatia Kanuni zetu za Kazi. Masuala yote kuhusiana na utii yapelekwe kwa msimamizi au meneja aliye karibu au meneja mkuu katika sehemu ya uendeshaji wa shughuli, ikiwa ni pamoja na masuala yanayohusu udanganyifu, wizi, ulaghai au utapeli, matumizi mabaya ya rasilimali za Kampuni, mienendo isiyo sahihi ya kiafya na kiusalama, rushwa, ufisadi au tabia nyingine yoyote iliyo kinyume na maadili ya mahali pa kazi.

Hata hivyo, kwa matukio ambapo si rahisi kuzungumza na msimamizi wako au meneja mkuu, kwa sababu yoyote ile, namba ya simu ya bure imetolewa katika kila nchi ambamo Xstrata inaendesha shughuli zake. Laini hiyo ya simu inaendeshwa kwa kujitegemea na KPMG, na mambo yote yatakayoripotiwa kwa njia ya simu yatapelekwa kisiri moja kwa moja kwa Mkuu wa Ukaguzi wa Mahesabu ya Ndani ili kuchukuliwa hatua zinazostahili. Unaweza pia kutumia anwani hii ya barua-e: ethics@xstrata.com.

Malalamiko, maswali, au migogoro inayohusiana na masuala ya rasilimaliwatu kama vile mishahara, saa za kazi, au majukumu, yataendelea kupelekwa kwa wasimamizi wenu, wafanyakazi au meneja wa rasilimaliwatu kama itakavyoonekana inafaa.

Ajentina	0800 555 5764	Papua New Guinea	050861140
Australia	1800 987 310	Peru	0800-5-2757
Belgium	0800 715 10	Philippines	1800 161 10175
Brazili	0800 890 069	Afrika Kusini	0800 20 43 07
Kanada	866 311 5773	Hispania	9005 06915
Chile	123 0020 9952	Uswazi	+27 12 543 5407
Jamhuri ya Dominika	888 751 0471	Uswisi	0800 000 998
Dubai	800 50 37283	Tanzania	+27 12 543 5449
Ujerumani	0800 18 13622	Uingereza	0800 0151 846
Norway	800 101 62	Marekani	1 800 988 1645

Baruapepe: ethics@xstrata.com

Maulizo ya Nje
Kwa maelezo zaidi kuhusu Xstrata, tafadhali wasiliana na:

Claire Divver
+44 20 7968 2871
cdivver@xstrata.com

Pamela Bell
+44 20 7968 2822
pbell@xstrata.com

Brigitte Mattenberger
+41 41 726 6071
bmattenberger@xstrata.com

www.xstrata.com

Lugha nyinginezo: kijitabu hiki kinapatikana pia katika lugha za Kiafrikaanasi, Kiingereza, Kifaransa, Kijerumani, Kinuktituti, Kinorwei, Kireno, Kisetswana, Kisepedi, Kisotho, Kihispania, Kiquechua, Kixhosa and Kizulu.

Kimesanifiwa & kutolewa na Cre8

Mixed Sources
Product group from well-managed forests, controlled sources and recycled wood or fiber
www.fsc.org Cert no. SGS-COC-1732
© 1996 Forest Stewardship Council
FSC

Kazi hii imechapishwa kwenye karatasi iliyoimarishwa ya 75. Karatasi imeidhinishwa kipekee kwa mujibu wa sheria za Forest Stewardship Council (FSC) na kupewa tuzo ya NAPM Recycled Mark. Imechapishwa St Ives Westerham Press Ltd, ISO14001, FSC certified and CarbonNeutral.®